

TANGAZO

Mfuko wa Udhhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania unatangaza nafasi za udhamini (Scholarships) wa masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2017/18.

Ufadhili huu, unalenga kuongeza hamasa na ufaulu kwa wanafunzi wa kike hapa nchini katika **masomo ya Hisabati na Sayansi**. Unajumuisha gharama zote za ada, pesa za kujikimu, mafunzo ya vitendo na vifaa vya kujifunzia ikiwemo kompyuta mpakato (Laptop). Utatolewa kwa wanafunzi sita raia wa Tanzania wenye ufaulu wa kiwango cha juu waliosajiliwa vyyo vikuu vinavyotambulika nchini.

Kwa **shahada ya kwanza**, ufadhili utatolewa kwa wanafunzi wenye ufaulu wa **Daraja la Kwanza miongoni mwa wanafunzi 10 bora kitaifa wa kidato cha sita mwaka 2017**, kwa masomo ya **Hisabati na Sayansi** kwa wanafunzi wa kike na kwa masomo ya **Uchumi, TEHAMA, Uhasibu na Fedha** kwa wanafunzi wa kike na wa kiume. Orodha ya wanafunzi kumi bora itaombwa moja kwa moja toka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

Kwa upande wa Shahada ya Uzamili, ufadhili utatolewa kwa wanafunzi wa kike na wa kiume waliofaulu kwa kiwango cha juu katika Shahada ya Kwanza kwa kozi za **Hisabati, Sayansi, Uchumi, TEHAMA, Uhasibu na Fedha**. Maombi yanakaribishwa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu udhamini huo na fomu za maombi tembelea tovuti ya BoT: www.bot.go.tz.

Fomu pia zinapatikana Benki Kuu Makao Makuu na katika Matawi ya Benki (Mwanza, Arusha, Zanzibar, Mbeya, Dodoma na Mtwara).

Limetolewa na:

Mwenyekiti,

Kamati ya Mfuko wa Udhhamini wa

Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere,

Benki Kuu ya Tanzania,

2 Mtaa wa Mirambo,

11884, DAR ES SALAAM.